# K.C.P.E 2ND PREDICTION

## DARASA LA NANE MWAKA -2022

## KISWAHILI {8}

*Muda: Saa 1 dak 40*

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:
   NAMBA YAKO YA MTIHANI

   JINA LAKO
   JINA LA SHULE YAKO
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano

Katika kijitabu cha maswali:

21. Kikosi ni kwa Askari ilhali kilinge ni kwa__________

A. wanakamati B. waimbaji
C. wachawi D. waumini

Jibu sahihi ni A

Katika karatasi ya majibu

1. [A] [B] [C] [D] 11. [A] [B] [C] [D] 21. [A] [B] [C] [D] 31. [A] [B] [C] [D] 41. [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Uchaguzi___1___ ambao ___2___kila baada ya miaka___3___ hapa nchini ni mojawapo ya___4___muhimu sana ya kidemokrasia.___5___wote waliofikisha___6___ya miaka kumi na minane ambao___7___kama wapiga kura hurauka mapema ili kuwachagua viongozi ___8___wale waliowapendeza kwa sera zao. Wakichagua viongozi wazuri sawa, wakichagua wabaya___9___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. mkubwa | B. mkuu | C. kuu | D. mdogo |
| 2. | A. unatendeka | B. ulifanyika | C. umejiri | D. hufanyika |
| 3. | A. mitano | B. tano | C. kumi | D. miwili |
| 4. | A. suala | B. jambo | C. mambo | D. jukumu |
| 5. | A. Raia | B. Watu | C. Wazalendo | D. Umma |
| 6. | A. umri | B. hirimu | C. mida | D. rika |
| 7. | A. walisajiriwa | B. watasajiliwa | C. wamesajiliwa | D. walisajiliwa |
| 8. | A. ... | B. ! | C. : | D. ; |
| 9. | A. ole wao! | B. hoiyee | C. makiwa | D. samahani! |

Bwana Manzo aliposimama ___10___, aliwarai wakazi wa___11___wa Majengo kumchagua kama ___12___wao ili awawakilishe kwenye___13___la kaunti. Shairi lake la ___14___ lilijaa sifa na wasifu kazi wake liliwasisimua wengi. Hata hivyo hakuwa na uhakika iwapo angechaguliwa na wanamajengo wote. Alijua___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. ulingoni | B. jukwaani | C. kizimbani | D. mimbarini |
| 11. | A. mtaa | B. eneo | C. jiji | D. kituo |
| 12. | A. gavana | B. seneta | C. diwani | D. rais |
| 13. | A. eneo | B. bunge | C. baraza | D. jopo |
| 14. | A. tarbia | B. tathitha | C. guni | D. utenzi |
| 15. | A. wengi wape | B. watu ni kikoa | C. kulenga si kufuma | D. bidii hulipa |

16. Neno Angushwa lina silabi ngapi?
A. 8 B. 7
C. 5 D. 3

17. Upi wingi wa sentensi
**Wakala alikuletea waraka wake**
A. Mawakala walimletea nyaraka zao
B. Wakala waliwaletea nyaraka zao
C. Mawakala walimletea waraka wao
D. Wakala walimletea nyaraka zenu.

18. Tegua kitendawili
**Yaenda mbali ila haiondoki ilipo**
A. mto B. macho
C. njia D. jua

19. Upi ukubwa wa sentensi ifuatayo.
Kikapu chenye maua kimeuziwa mzee
A. Kapu lenye majiua limeuziwa jizee
B. Jikapu lenye majua limeuziwa zee
C. Kapu lenye majijua limeuziwa jizee
D. Jikapu lenye majijua limeuziwa jizee

20. Ni nini maana ya sentensi zifuatazo
Karani aliandika barua. Karani alikuwa ofisini
A. Karani aliandika barua kwa ofisi
B. Barua iliandikiwa karani ofisini
C. Karani aliandikiwa barua ofisini
D. Barua iliandikwa na Karani akiwa ofisini

21. Chagua nomino iliyoundwa kutokana na kitenzi
A. Saka - msusi
B. Tiba - tabibu
C. Tubu - toba
D. Tii - tiifu

22. Chagua sentensi sahihi na mantiki
A. Hoyee! Tumeshindwa na shule yetu.
B. Hewala! Nitakupeleka mjini leo jioni.
C. Kichungi cha chai kimechomeka.
D. Dhana ya uhifadhi wa mazingira sio geni.

23. Sayari iliyo kubwa zaidi kuliko zote ni
A. Zohali B. Mirihi
C. Mshtarii D. Zaibaki

24. Chagua fungu lenye nomino za ngeli moja
A. Ubele, uyoga, uta
B. Maji, marashi, mawe
C. Ulezi, uteo, uzi
D. Wenzo, ua, ubeleko

25. "Kombe la dunia litawaniwa baadaye mwaka huu." Mwalimu alisema katika usemi taarifa itakuwa.
A. Mwalimu alisema kuwa kombe la dunia lingewaniwa baadaye mwaka huo.
B. Mwalimu alisema kombe la dunia litawaniwa baadaye mwaka huu
C. Mwalimu alisema kuwa kombe la dunia litawaniwa baadaye mwaka huo
D. Mwalimu aliahidi kuwa kombe la dunia litawaniwa baadaye mwaka huu.

26. Chagua maelezo sahihi
A. Kisugudi ni sehemu ya nyuma ya mguu.
B. Kitengele ni sehemu ya mkono yenye vidole
C. Panda ni sehemu baina ya kiuno na goti
D. Utosi ni sehemu ya nyuma ya kichwa

27. Bainisha maneno yaliyopigiwa kistari.
Baba aliegesha gari <u>kwa</u> jirani, <u>kwetu</u> kumejaa <u>pomoni</u>.
A. Kihusishi, kiwakilishi, kielezi
B. Kiunganishi, kimilikishi, Nomino
C. Kielezi, kiwakilishi, kielezi
D. Kiunganishi, kiwakilishi, kielezi

28. Ukuta ni kwa timazi kama vile sakafu ni kwa ________
A. mahati B. utepe
C. mizani D. pimamaji

29. Tupa ni kuacha bila ya uangalizi, tupa pia ni
A. kutenga vitu mahali
B. kumpa mtu kitu usichohitaji
C. chombo cha chuma cha kunolea
D. chombo cha chuma cha kukatia

30. Aisifuye mvua imemnyea ni kwa wanaokisifu kitu wanachokijua vizuri ilhali hauendi ua kwa nyenzo ni kwa
A. wanaodharau vitu vidogo vidogo
B. wanaotafuta namna ya kufanya jambo
C. wanaoona shida za wengine kuwa ndogo
D. wanaodharau waliowasaidia awali

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31- 40**

Kuna msemo kwamba, "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo." Ni dhahiri kwamba adinasi wengi hufungamanisha maana ya ulumbi huu na jinsi mtoto anavyokuzwa na mvyele au mlezi wake.

Ni muhimu kuufasiri usemi huu kwa mapana zaidi. Jinsi jamii inavyomwandalia mtoto mazingira ndivyo anavyoathiriwa na mazingira yayo hayo. **Mtoto ni mtoto, yeye huiga watu wazima na kufuata mkondo anaolekezwa aufuate.** Hafuati mzazi tu bali jamii nzima inayomfinyanga katika kukua kwake kimwili, kiafya, kifikra, kiutu na kimaadili kwa jumla.

Mojawapo ya athari za kukua kwa mtoto kulikokamilika ni ajira za watoto. Kwao watoto ni rasilimali ya kutumiwa kuendeleza majukumu mbalimbali kama vile kutema kuni, kuvuna mazao kama vile chai, pareto na kahawa, kulisha mifugo na kazi nyingine kochokocho ambazo katu hazistahili kufanywa na mtoto.

Ajira za watoto ni dhuluma dhidi yao. Kwanza, watoto hawajakomaa kimwili kuzimudu gange hizo. Kwao ni kazi za sulubu. Pili, wananyimwa haki ya kushughulikia mambo yanayoambatana na umri wao yakiwemo elimu na michezo. Watoto hawapati nafasi ya kujumuika na wenzao, kucheza, kupendwa na kutunzwa kwa kuzingatia mahitaji yao kama watoto.

Matatizo ya watoto ni mengi na huathiriwa na masuala ya kijinsia. Mabinti wanashida nyingi kutokana na mielekeo ya kijamii. Tamaduni nyingi kote duniani zimempuuza mwanamke kwa muda mrefu. Wasichana wameendelea kunyimwa nafasi ya kusoma. Baadhi yao huozwa wangali wachanga. Gashi hufanyishwa shughuli nyingi kama vile kufua, kulea, kubeba mitungi ya maji na majukumu mengine katika miktadha ya kuajiriwa. Hali hizi za kusikitisha haziwaruhusu kuendelea na masomo ipasavyo.

Watoto wakosapo élimu huwa hawakui vizuri kimawazo wala hawawezi kuchangia kikamilifu katika harakati za ujenzi wa jamii ya kisasa wanapaswa kuelewa mambo ya kidijitali, yaani matumizi ya vyombo vya kielektroniki mathalani simu na tarakilishi. Elimu wanayopewa watoto shuleni inazingatia vyema miktadha yote ya kimaendeleo katika jamii. Maendeleo haya hayawezi kamwe kufanikiwa iwapo watoto watazidi kudidimizwa katika ajira

Juhudi zinazofaa kufuatiliwa ni zile zitakazowajenga vijana wala si kuwabomoa. Ni lazima ajira za watoto zishtumiwe vikali na raia wote na serikali pia ili watoto waviepuke vikwazo hivyo vinavyowalemaza.

Watoto wana haki ya kuzijua haki zao. Wana haki ya kukataa kudhulumiwa. Pia wanahaki ya kutokubali kufanya kazi za ajira. Haki za watoto ni haki za kibinadamu.

31. Kulingana na aya ya kwanza
A. jukumu la malezi ni la mzazi peke yake
B. hulka ya mtoto huathiriwa na malezi aliyopokea udogoni
C. watu wanaelewa vizuri maana ya methali za malezi
D. watu wengi hawajui jinsi walivyolelewa na wazazi

32. Chagua kauli isiyo sahihi
A. Mazingira mwafaka humfanya mtoto awe mwadilifu.
B. Mazingira duni huwa na athari chanya kwa mtoto.
C. Malezi ya mtoto ni dhima ya wanajamii wote.
D. Ukuaji wa mtoto huegemea mikondo tofauti tofauti.

33. Ni methali gani inayoambatana na kifungu kilichoangaziwa katika aya ya pili?
A. Mtoto ni kito lakini mzigo mzito
B. Mwana mui ni dawa ya mlango
C. Tajiri na mali yake maskini na mwanawe
D. Mtoto akibebwa hutazama kisogo cha nina

34. Madhara makuu ya ajira ya watoto ni kuwa
A. huathiri kukua kwa mtoto kulikokamilika.
B. huwanyima nafasi ya kutangamana na wenzao
C. watoto huanza kufanya kazi mapema
D. serikali imeharamisha kitendo cha kuajiri watoto

35. Haki za mtoto zinazokiukwa anapoajiriwa ni
A. elimu na uhai
B. ushirika na lishe bora
C. mavazi na elimu
D. mapenzi na elimu

36. Kwa nini watoto wajinsia ya kike wanakabiliwa na changamoto nyingi kuliko wenzao wa kiume?
A. Wasichana hawana nguvu kama watoto wa kiume.
B. Watoto wa kiume hubaguliwa zaidi katika jamii
C. Desturi za jamii nyingi humdunisha mtoto wa kike
D. Wanajamii wengi hawamthamini mtoto wa kiume.

37. Dhima ya elimu katika jamii ni
A. kuwawezesha watoto kutangamana na kutumia mitambo mbalimbali
B. kuwakuza watoto kimawazo na kuchangia maendeleo ya jamii
C. kujifunza taaluma mbalimbali na kuiletea jamii sifa
D. kujipatia ajira na kutetea ubaguzi wa kijinsia

38. Ajira ya watoto itakabiliwa ipasavyo na
A. watoto na wavyele
B. serikali na waajiri
C. serikali na wazalendo
D. wazazi na walimu.

39. Kwa vyovyote vile, mwandishi hasemi kwamba
A. watoto wasifanyishwe kazi
B. wasichana wengine wanadhalilishwa
C. haki za watoto zinaendelea kukiukwa
D. watoto wanapaswa kuzifahamu haki zao

40. Kisawe cha neno dhuluma kama lilivyotumika ni
A. uchochezi B. onea
C. uonevu D. kandamiza

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kutoka 41- 50**

Naikumbuka siku hiyo vizuri. Niliamka alfajiri mbichi tayari kuelekea mjini ambako nilikuwa na wingi wa matumaini ya kupata mshahara wangu wa kwanza tangu nilipoajiriwa. Baada ya kumaliza masomo vibao vya 'hamna kazi' vilinilaki kila wakati. Baadaye nikabahatika kama mwana aliyepokelewa kwa kipini cha dhahabu mkononi. Hamu na hamumu ilijikita moyoni baada ya siku thelathini ili kupata jasho langu na kutimiza matakwa yangu ya kibinafsi na ya kifamilia.

Taraa nilipowasili katika benki nilipata safu ya wateja waliohudumiwa. Tafakurini nilikuwa na mawazo walakini yote yalikuwa ya kuvutia. Nilikuwa na mipango kabambe kuhusu mshahara wangu wa kwanza. Kwa mfano nilipania kununua suti maridadi ya sufu ya kondoo, viatu vya ngozi ya chatu na mavazi mengine ya kuvutia. Pili ningenunua vinono vya kuipelekea jamaa yangu iliyonisaidia kwa hali na mali wakati nilipokuwa nikijiendea shambiro bila kazi yoyote. Yakini si yamkini, damu ni nzito kuliko maji.

Baada ya robo saa nikiwa kwenye safu ikawa ni nafasi yangu ya kuhudumiwa. Hali ilikuwa shwari na bambam minghairi ya shari. Unyamavu na makuburi ukashika hatamu wakati mhudumu wa benki alipokuwa akinihudumia. Mabarobaro wanne waliojihami kwa silaha ghushi walijitoma ukumbini huku wakiwa wamejikwatua kwa suti maridadi walitoa amri kila mja kulala kwa tumbo. Tayari kibindo changu kilikuwa kiunoni.

Ghafla bin vuu hali ya vurumai ilitanda katika ukumbi wa benki. Waliojifanya kuwa wateja kumbe walikuwa majambazi. Washika doria waliokuwa kwenye milango ya tarabe ya benki walifungwa kifati wasiweze kufurukuta. Kiongozi wa genge lile alitoa kauli kila mja asithubutu kuongea au kupiga hatua yoyote. Kimya cha makaburi kikashitadi wakati jambazi mmoja alipompiga risasi mteja aliyekuwa nyuma kwa kukiuka sheria zao.

Baada ya kitambo kidogo, tulikuwa tumeporwa pesa zote na vitu vyenye thamani kama saa, rununu, mikufu na kadhalika. Ama hakika mshahara wangu wote ulitwaliwa na jitu lile lisilo na huruma wala imani. Niligumiwa na hali ile nikajipata nikijiuliza maswali ya balagha; wizi au mazingaombwe? Wizi wa mchana wakati wa jua la mtikati au la? Hatimaye nilipiga milundi hadi nyumbani bila hata nauli ya kusafiri. Matumaini ya kutumia mshahara wangu wa kwanza, yakadidimia kama taa ya kibatari iliyotumbukizwa majini. Hadi leo nisimuliapo kisa hiki, suala hili limebaki kuwa kitendawili na wakukitegua hajapatikana. Kweli wasemao walilenga ndipo kwamba, 'usikate mbeleko kabla ya mwana kuzaliwa.' Aidha kulenga si kufuma. Mtume! Aliyeumwa na nyoka aonapo kamba hushtuka.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

41. Kulingana na msimulizi;

A. Alipata kazi pindi tu alipohitimu masomoni

B. Alidhurika kabla ya kupata kazi

C. Alijinunulia suti na viatu vya kipekee

D. Alipanga kujinufaisha pekee kutokana na mshahara ule

42. Chagua jibu sahihi kuhusu benki kwa mujibu wa kifungu hiki

A. Wateja waiihudumiwa bila ya safu

B. Milango ya benki ilikuwa ya chuma na pia ya kudumu

C. Msimulizi hakuwa amehudumiwa wakati ujambazi ulipotekelezwa

D. Haukuwa wizi bali mazingaombwe ya wakazi wa miji

43. Matumaini ya kupata mshahara wa kwanza yalimfaa msimulizi

A. kuwa na mawazo ya kusononesha

B. kuwa na mawazo ya kujisahau

C. kuwa na mseto wa furaha na jitimai

D. kuwa na mawazo ya kufurahisha

44. Kulingana na ufahamu, wateja kwa wahudumu waliagiziwa kulala kwa tumbo, huku ni kulala

A. kingalingali B. chali

C. kifudifudi D. kidari

45. Msimulizi alikuwa amehifadhi pesa katika

A. mfuko mdogo ndani ya shati

B. mfuko mdogo mbele ya suruali

C. mkunjo mdogo ulioshonewa kiunoni

D. mkunjo wa nguo uliofungwa kiunoni

46. Mfuatano upi wa matukio ni sahihi

A. kusoma, kuhitimu, kuhojiwa, kuajiriwa

B. kuhitimu, kusoma, kuajiriwa, kuhojiwa

C. kuajiriwa, kusoma, kuhojiwa, kuhitimu

D. kusoma, kuhojiwa, kuhitimu, kuajiriwa

47. Washika doria "walifungwa kifati" kulingana na ufahamu ina maana

A. kufungwa mwili wote

B. kufungwa mikono pekee

C. kufungwa mikono na miguu

D. kufungwa miguu na midomo

48. Hamu ya mwandishi ya kutumia mshahara wake wa kwanza ilizidi kadri

A. nguvu zake za kufanya kazi zilivyoendelea kudidimia

B. siku za mwezi zilivyoendelea kuyoyoma

C. majambazi walivyoendelea kupora wateja wengine

D. vishindo katika benki vilivyokita

49. Chagua jibu lisilo sahihi kulingana na kifungu

A. Majambazi walikuwa miongoni mwa wateja wengine.

B. Majangili walikuwa wamejificha ukumbini.

C. Msimulizi hakuamini uhalifu ulitendeka kwenye benki

D. Matumaini ya kutumia mshahara yaliisha pindi uhalifu ulipotekelezwa.

50. Funzo la msimulizi kutokana na methali zilizotumika ibara ya mwisho hii ni

A. tusiwe watu wa kupangia vitu kabla wakati hujawadia

B. tupangie vitu vyetu vizuri

C. tusiwe watu wa kupangia vitu vyovyote

D. tujifunze kuhifadhi vitu vyetu vilivyo



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com